

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

**MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI KWA
KIPINDI CHA NOVEMBA 2016**

Dondoo muhimu za mwezi Novemba, 2016

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2016 na mwelekeo wa viashiria vya mifumo ya hali ya hewa pamoja na mvua katika kipindi cha mwezi Novemba, 2016.

- a. Mwelekeo wa mvua za Vuli, 2016 kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2016:
Hali ya upungufu wa mvua inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi katika kipindi cha mwezi Novemba, 2016.
- b. Maeneo ya Nyanda za juu Kaskazini mashariki pamoja na maeneo ya mkoa wa Tabora mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2016.
- c. Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, na mvua za chini ya wastani katika maeneo mengine ya nchi.

1. MUHTASARI WA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA, 2016

Kipindi cha mwezi Oktoba, 2016 mvua zilichelewa kuanza katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, hali iliyosababisha upungufu mkubwa wa unyevunyevu katika maeneo mengi ya nchi. Maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan yale ya Ziwa Victoria yalipata mvua za chini ya wastani katika kipindi cha mwezi Oktoba. Takwimu zinaonyesha kuwa kuanzia mwishoni mwa mwezi Septemba, 2016 hadi sasa kumekuwa na hali ya upungufu wa mvua na mtawanyiko wake ulikuwa hafifu katika maeneo mengi.

2. MWELEKEO WA MVUA NOVEMBA, 2016

2.1 Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Hali ya ukavu na vipindi vifupi vya mvua inatarajiwa hususan katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2016. Hali ya joto inatarajiwa kuongezeka katika kipindi hicho. Mvua zinatarijiwa kuwa chini ya wastani katika kipindi hiki.

2.2 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Hali ya ukavu na vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa kuanza wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2016. Mvua zinatarijiwa kuwa chini ya wastani katika kipindi hiki.

2.3 Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Mvua za wastani zitakazoambatana na ngurumo zinatarijiwa katika baadhi ya maeneo. Mvua zinatarijiwa kuwa za wastani katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria na chini ya wastani katika maeneo mengi.

2.4 Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua zitakazoambata na ngurumo katika maeneo machache zinatarijiwa. Mvua zinatarijiwa kuwa chini ya wastani, hata hivyo mkoa wa Tabora unatarajiwa kuendelea kuwa na hali ya ukavu hususan katika kipindi cha mwazoni mwa mwezi Novermba 2016.

2.5 Kanda ya kati ya nchi (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu na joto itakayoambatana na vipindi vichache vya upepo mkali.

2.6 Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Njombe, Iringa na Mbeya region): Hali ya ukavu kwa ujumla na mvua chache katika maeneo machache hususan ya miinuko inatarajiwa.

2.7 Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Hali ya ukavu kwa ujumla, joto na mvua chache katika maeneo machache zinatarajiwa. Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza.

2.8 Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Hali ya ukavu kwa ujumla na mvua chache hususan katika maeneo ya miinuko. Vipindi vifupi vya upepo makali vinatarajiwa katika maeneo ya Ziwa Nyasa.

Izingatiwe kuwa pamoja na kuwapo kwa mvua chache (chini ya wastani) uwezekano wa matukio ya vipindi vya mvua kubwa pia yanaweza kujitokeza .

3. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Upungufu mkubwa wa unyevunyevu unaonekana kuendelea katika maeneo mengi ya nchi kutokana na kuendelea kuwepo kwa viashiria vya kupunguza mvua kama La Nina na joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi. Hata maeneo ya magharibi mwa nchi ambapo unyevunyevu unatoka katika misitu ya Congo pia kunatarajiwa kuwa na upungufu wa unyevunyevu kutokana na joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na Pwani ya Angola. Ukanda wa mvua (ITCZ) ambao ulisogea katika eneo la kaskazini mwa nchi za Africa mashariki unaonekana kufifia hususan katika eneo la mashariki mwa nchi. Hata hivyo ITCZ katika kipindi cha mwezi Novemba, 2016 inaonekana kusogea taratibu kuelekea kusini mwa Ikweta.

Imetolewa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Dkt. Agnes L. Kijazi